JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BENKI KUU YA TANZANIA

**22 Novemba 2025**

## TAARIFA KWA UMMA

## UPOTOSHAJI WA KUTOKEA KWA SHAMBULIO LA KIMTANDAO KATIKA BENKI NCHINI

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kukanusha taarifa za upotoshaji kuhusu usalama wa mifumo ya malipo na akaunti za amana katika benki na taasisi za fedha hapa nchini. Taarifa hizo potofu zinahamasisha wateja wenye amana kwenye benki za biashara kuondoa fedha zao kwa maelezo kuwa mifumo ya benki itashambuliwa na wahalifu wa kimtandao, hivyo kusababisha upotevu wa fedha za wateja na kutopatikana kwa huduma za kibenki.

Benki Kuu inawahakikishia wananchi kuwa mifumo ya malipo ya Taifa pamoja na amana za wateja katika benki za biashara ni salama na inaendelea kuzisimamia kwa ufanisi na tija inayostahiki.

Vilevile, wananchi wanashauriwa kuendelea kutunza amana zao katika benki kwani kuna manufaa mengi, yakiwemo pesa kuongezeka kutokana na malipo ya riba au faida ya mwaka, fedha kutunzwa kwa usalama, na uwepo wa bima ya amana endapo benki itafilisika. Aidha, amana za wateja zinawezesha benki kutoa mikopo kwa wananchi wanaohitaji mitaji, hivyo kuchangia kukuza Uchumi wa mtu mmoja mmoja na Uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Benki Kuu inawaonya wote wanaosambaza taarifa hizo mitandaoni kuacha mara moja, kwani tabia hiyo haina tija katika maendeleo ya sekta ya fedha, uchumi wa mtu mmoja mmoja au uchumi wa taifa kwa ujumla. Benki Kuu kwa kushirikiana na vyombo vya sheria, itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeendelea kueneza taarifa hizi za upotoshaji.

**Emmanuel M. Tutuba**
**GAVANA**

16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501